102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
JUNI 2013
Muda: Saa 2½

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Saa 2½

Maagizo:

- Jibu maswali **manne** pekee.
- Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki-**Hadithi Fupi, Tamthilia, Ushairi** na **Fasihi Simulizi.**
- Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja.**
- Maswali yote yana alama sawa.

	SEHEMU	UPEO	TUZO
A.	UTENGANO	20	
B.	DAMU NYEUSI	20	
C.	MSTAHIKI MEYA	20	
D.	USHAIRI	20	
E.	FASIHI SIMULIZI	20	
	JUMLA	80	

SEHEMU A: RIWAYA

SWALI LA LAZIMA

UTENGANO: S. A MOHAMED (ALAMA 20)

1. "Dunia ni sumu, yafaa utahadhari.'
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

   (b) Fafanua sifa mbili za msemaji na msemewa. (al.4)

   (c) Tambua mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili, kisha utoe maelezo yake.(al.2)

   (d) Kwa kurejelea riwaya hii, jadili ukweli wa kauli hii. (al.10)

SEHEMU B: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI- KEN WALIBORA NA S. A. MOHAMMED

2. "….Alinihakikishia shughuli yote ingekamilika vizuri. Nilielewa fika chochote kingeweza kutokea. Mwiba wa kujidunga…"

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

   (b) Eleza sifa tatu za msemaji. (al. 6)

   (c) Tambua mbinu mbili za lugha zinazorejelewa katika dondoo hili. (al. 2)

   (d) Onyesha namna mwandishi wa hadithi husika alivyoshughulika matumizi ya jazanda. (al.8)

3. Huku ukirejelea hadithi zozote **tano** katika diwani ya 'Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine' fafanua namna mwanamke alivyosawiriwa. (al. 20)

SEHEMU C:TAMTHILIA

MSHTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE

3. "…nikumbushe tena na tena mpaka apate mwanga wa kile unachokisema."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)

   (b) Fafanua sifa sita za anayesema maneno haya. (al 6)

   (c) Maudhui yafuatayo yamefafanuliwaje katika tamthilia ya Mushtahiki Meya. (al 10)
      (i) Udhalimu
      (ii) Unafiki

4. Thibitisha jinsi tamthilia ya ‘Mshtahiki Meya’ inavyoafiki jamii ya kisasa. (al 20)

SEHEMU YA D: SHAIRI **(alama 20)**

Nimechoka
Nilivyofikisha hapa, na juu kupandishwa
Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha,sijui.

Wanadamu wameinama.Wanasali kwa haraka sasa.
Utafikiri wanahesabu mchanga utakaojaza kaburi langu.
Vichwa vyeupe vinacheka. Kingine kinasema tena:
“Mnaliona Hilo! Joga !” Vichwa vinachela. Wanasali.
“Nyinyi nyote hamna akili! Mnaniudhi!
Hamwoni hali yangu!” Napiga kelele. Lakini vichwa
Havitishi, na wanadamu hawatingishiki.

Sauti ya baba inasema kwa msisitizo
“Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka.
“Lakini unazo nguvu bado, na usikate tamaa,
Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa;
Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,
Nawe kudondoka, utadondoka!

Ninaendela kuning’inia. Nimechoka. Mikono
Inaniuma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali
Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao; maana
Mimi bado nimeniong’inia na vitimbo having’oki.
Lakini pole pole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijadondoka

Lakini najiona nimening’inia kama ndege
Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo
Mimi, lakini ni mwanadamu na akili zangu
Timamu. Ninaweza kudondoka, kama nikipenda.

Lakini ninaogopa chini yangu naona miti
Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
Ikingoja kwa hamu, kama mshikaki kunichoma,
Kunitoboa na kufurahia kimya kimya,
Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu.
Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurushi
Cha pamba cha mtoto mdogo kilichokwisha pimwa.

Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.
Nimechoka. Kadiri niendelavyo kuning'inia, ndivyo
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma.
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!

Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani, itingishike kuwatisha
ndege.
Machozi yananitoka, kuyapangua siwezi.
Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu;
"Jamani e! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!"
Lakini wanadamu wameinama. Wanaanza sasa kusali.

Kati ya vitimbo, vichwa vinazuka ardhini
Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo.
Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "Mnaliona Hilo!"
Halafu vichwa vyote vyeupe vinacheka. Ninashangaa.
Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba
Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe.
Siyaamini macho,siyaamini masikio,sikiamini kichwa.

Maswali:

1. Shairi hili ni la udhanaishi" fafanua kauli hii. (al. 4)

2. Eleza kwa kutoa mifano miwi;li miwili, jinis msanii alivyotumia tamathali zifuatazo: (al. 6)

   (a) Jazanda

   (b) Uhuishi

   (c) Taswira

3. Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. (al 4)

4. Eleza maana ya mshororo "vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo, nawe kudondoka utadondoka". (al 2)

5. Eleza umbo la shairi hili. (al 4)

5. FASIHI SIMULIZI **(ALAMA 20)**

(a) Taja na ueleze vipera ya maghani. (al 10)

(b) Eleza hatua muhimu za utafiti na ukusanyaji data kata\ika fasihi simulizi. (al 10)